**MKATABA WA HUDUMA YA UFUNDI WA UJENZI WA KAMBI YA UTALII (CAMPSITE) KATIKA PORI LA AKIBA LUKWIKA**

**KATI YA**

**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA (TAWA)**

**NA**

**GEORGE E. MPONDA**

**DECEMBER 2021**

**MKATABA WA HUDUMA YA UFUNDI WA UJENZI WA KAMBI YA UTALII (CAMPSITE) KATIKA PORI LA AKIBA LUKWIKA**

Mkataba huu umeingiwa leo tarehe 30 Mwezi Desemba mwaka 2021, **BAINA** ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – yenye ofisi yake eneo la Barabara ya Dar es salaam, Jengo la TAFORI Eneo la Kingolwira ,

S.L.P .o. Box 2658, Morogoro. (hapa ataitwa 'TAWA'-HQ ) kwa upande mmoja.

**NA**

Ndugu **GEORGE ETIENE MPONDA** wa Masasi- **Mtwara** ambaye kwa mkataba huu (ataitwa 'mjenzi') kwa upande wa pili.

**1. UTANGULIZI**

**TAWA** ni Taasisi ya Serikali inayojitegemea Iliyoanzishwa chini yaSheria ya kuhifadhi Wanyamapori No.5 ya Mwaka 2009, kusimamia Wanyamapori wanaopatikana nje ya Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Eneo la Ngorongoro ambayo inatekeleza miradi yake mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa njia ya waenda kwa miguu katika Pori la Akiba la Mpanga Kipengere, mapolomoko ya Lyamanohila

**Mjenzi** ni Mwenye utaalam wa kujenga Majengo na ukarabati wa miundo mbinu mbalimbali ambaye anamiliki kikundi cha ufundi chenye ujuzi na uzoefu wa kazi husika.

**TAWA** iko tayari kumpatia Mjenzi kazi za utendaji pekee (labour only) ili afanye kazi yote ya kukarabati hadi kukamilisha kazi zote tajwa katika mkataba huu kama itakavyoainishwa.

**Mjenzi** ameona kazi husika na kuelewa ukubwa na mahitaji ya kazi ikiwa ni pamoja na ubora unaotakiwa (Specification).

**2. Ukubwa wa kazi (Scope of works).**

| Na. Mfululizo | Maelezo ya Kazi |
|---|---|
| 1 | Kusafisha eneo la kazi |
| 2 | Kuchimba na kuondoa udongo wenye rutuba kina kisichozidu milimita 150 |
| 3 | Kuchimba mashimo ya nguzo kina kisichozidi mita moja na nusu |
| 4 | Kuchimba msingi wa nyumba kwa kina kisichozidi mita moja na nusu |
| 5 | Kurudisha udongo uliochimbwa kwa kutumia kifusi kichopendekezwa |

| | |
|---|---|
| | na wataala na kushindilia kote |
| 6 | Kupakia na kuondoa udongo uliochimbwakutoka eneo la ujenzi |
| 7 | Kupanga mawe kwenye jengo kabla ya kumwaga jamvi |
| 8 | Kupiga dawa ya kuua wadudu aina ya gammalin sultion |
| 9 | Kupiga dawa ya kuuwa wadudu aina ya gamalin solution |
| 10 | Kupiga dawa ya kuuwa wadudu aina ya gamalin solution |
| 11 | Kutandaza karatasi la Nailon kuzuia unyevu kupanda juu ya msingi |
| 12 | Kusuka nondo za nguzo na mikanda bimu |
| 13 | Kupiga mbao za fomu weki kwenye nguzo kwa ajili ya kumwaga zege |
| 14 | Kupiga mbao za fomu weki kwenye nguzo kwa ajili ya kumwaga zege |
| 15 | Kupiga mbao za fomu weki kwenye nguzo kwa ajili ya kumwaga zege |
| 16 | Kupiga mbao za fomu weki kwenye nguzo kwa ajili ya kumwaga zege |
| 17 | Kupiga fomu weki kwenye ngazi |
| 18 | Kujenga ukuta wa jingo wenye unene wa 230mm |
| 19 | Kujenga kozi kwa ajili ya kuzuia unyevu kupanga kwenye kuta za nyumba |
| 20 | Kupiga plasta kwa ajili ya rangi ya mafuta unene wa 15mm |
| 21 | Kupiga rangi kwenye kuta za jengo |
| 22 | Kumwaga zege kwenye jengo |
| 23 | Kujenga ukuta wa tofali wenye unene wa 150mm |
| 24 | Kujenga kuta za ndani patisheni kwenye jengo |
| 25 | Kupiga bati geji 28 kwenye jengo |
| 26 | Kuweka kofia kwenye paa/bati zenye unene wa 30mm |
| 27 | Kupiga mbao za kenchi |
| 28 | Kuweka Milango kwenye jengo |
| 29 | Kuweka frame kwenye jengo |
| 30 | Kuweka madirisha kwenye jengo |
| 31 | Kupiga plasta kwenye jengo |
| 32 | Kuweka tiles kwenye jingo ukutani na chini |
| 33 | Kuweka mikanda ya marumaru kwenye ukuta |
| 34 | Kuweka ukanda wa chuma kwenye ukuta |
| 35 | Kuweka ukanda wa chuma kwenye ukuta |
| 36 | Kupiga gypsum kwenye paa la jengo |
| 37 | Kupiga mbao za blandaring |
| 38 | Kupiga siling bodi kwenye paa la nje |
| 39 | Kuweka mikanda kwenye gypsum |
| 40 | Kuweka udongo wenye unene wa 9mm kwa ajili ya kupokea marumaru |
| 41 | Kuweka vyoo kwenye jengo |
| 42 | Kuweka bomba za maji safi na taka kwenye jengo |
| 43 | Kuchimba na kujenga shimo la maji taka/choo |
| | |
| | |

| | |
|---|---|
| | |
| 1 | Kusafisha eneo la kazi |
| 2 | Kuchimba na kuondoa udongo wenye rutuba kina kisichozidu milimita 150 |
| 3 | Kuchimba mashimo ya nguzo kina kisichozidi mita moja na nusu |
| 4 | Kuchimba na kuondoa miamba |
| 5 | Kurudisha udongo uliochimbwa kwa kutumia kifusi kichopendekezwa na wataala na kushindilia kote |
| 6 | Kupakia na kuondoa udongo uliochimbwakutoka eneo la ujenzi |
| 7 | Kupanga mawe kwenye jingo kabla ya kumwaga jamvi |
| 8 | Kupiga dawa ya kuua wadudu aina ya gammalin sultion |
| 9 | Kupiga dawa ya kuuwa wadudu aina ya gamalin solution |
| 10 | Kumwaga zege |
| 11 | Kusuka nondo za nguzo na mikanda bimu |
| 12 | Kupiga mbao za fomu weki kwenye nguzo kwa ajili ya mkanda wa linta |
| 13 | Ujenzi wa ukuta wa tofali |
| 14 | Kujenga kozi kwa ajili ya kuzuia unyevu kupanda ndani ya jingo yenye unene wa 230mm |
| 15 | Kujenga plasta kwenye kuta |
| 16 | Kupiga rangi kwenye kuta za jengo |
| 17 | Ujenzo wa kuta kwa tofali wenye unene wa 150mm |
| 18 | Kupiga mbao za kenchi |
| 19 | Kupiga bati geji 28 |
| 20 | Kuweka bomba za maji safi na maji taka |
| 21 | Kupachika frame na milango |
| 22 | Kupachika grill na madirisha ya aluminium |
| 23 | Kupiga plasta ya kioo |
| 24 | Kuweka floor kwa ajili ya kupokea marumaru |
| 25 | Kuweka marumaru kwenye kuta na floor |
| 26 | Kuweka udongo kwa ajili ya kupokea mikanda ya tiles |
| 27 | Kuweka marumaru kwenye jengo |
| 29 | Kuweka marumaru kwenye kuta na floor kuweka udongo kwa ajili ya kupokea mikanda ya tiles |
| 31 | Kuweka mikanda ya marumaru kwenye kuta |
| 32 | Kupiga siling bodi kwenye paa |
| 33 | Kupiga mbao za blandaring |
| 34 | Kupiga rangi kwenye kuta zilizopigwa rangi na kwenye gypsum |
| 35 | Kupiga msasa na vanish kwenye milango |
| 36 | Kujenga karo la choo |
| 37 | Kupachika vyoo kwenye jengo |
| 38 | Kuweka vioo vya kujiangalizia chooni |

## 3. SASA INAKUBALIKA KWA PANDE ZOTE KAMA IFUATAVYO:

### A. MALIPO

TAWA itamlipa mjenzi jumla ya Shs. **21,000,000/=** (Shilingi za **kitanzania Milioni Ishirini na Moja tu) zitakazolipwa kwa awamu mbili.**

1. Malipo ya awali asilimia 60% (**TZS. 12,600,000/=) Milioni kumi na mbili na laki sita )** zitakazolipwa ndani ya siku saba (7) baada ya kusaini mkataba huu na kuanza kazi.
2. Malipo ya pili na ya mwisho asilimia 40 % **(TZS. 8,400,000/=) Milioni Nane na laki nne)** zitalipwa baada ya kazi kukamilika.

### B. MUDA

Muda wa kutekeleza mradi huu ni siku Tisini (90) ikijumlisha pia siku za mwisho wa juma. Muda wa kumaliza kazi unaibana TAWA na Mjenzi na hivyo mjenzi anatakiwa kufanya kazi tajwa bila kusimama. Mjenzi atasimamisha kazi endapo vifaa vya ujenzi (building materials) vitakuwa vimeisha au hali ya hewa kutoruhusu kufanyika kwa kazi.

### C. VIFAA VYA UJENZI (BUILDING MATERIALS)

TAWA itawajibika kuleta vifaa vya ujenzi (building materials) vinavyohitajika kwa wakati kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kambi ya Utalii (campsite) katika Pori la Akiba la Lukwika.

Vifaa vyote vitafikishwa eneo la ujenzi, Kutokuwepo kwa vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kazi itakuwa sababu mojawapo ya mjenzi kusimamisha kazi.

### D. USIMAMIZI WA UJENZI.

Kutakuwa na msimamizi wa mjenzi. Kwa kuwa kazi hii ni ya TAWA msimamizi wa ubora wa kazi atatoka TAWA. Msimamizi atakuwa akitoa maelekezo juu ya utendaji kazi ili kupata ubora unaohitajika na kwamba atakuwa akishauriana na Mjenzi juu ya ubora wa ujenzi. Msimamizi pia atakuwa na jukumu la kutunza muda wa mradi. Utunzaji wa muda utahusu kujadiliana na mjenzi juu ya hatua stahiki za kufanya ili kazi isichelewe kutokana na mpango kazi wa mradi.

## E. MITAMBO.

Pale itakapohitajika, Tawa itatoa vifaa ili kukamilisha mradi kwa wakati. Mjenzi atawajibika kutoa mahitaji hayo mapema ili maandalizi yafanike kwa wakati

## F. USALAMA KAZINI.

Mjenzi atawajibika kwa masuala yote ya usalama kazini. Hii itajumuisha usafi wa eneo la mradi ikiwa ni pamoja kuhifadhi na kutunza mazingira ya eneo husika.

## G. KUTUNZA VIFAA

Vifaa vyote kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi huu vitatunzwa na mtunza stoo wa TAWA. Mtunza stoo atakuwa na jukumu la kuhakikisha usalama wa vifaa vyote vinavyotumika kwenye ujenzi.

## H. KUCHELEWA KWA MALIPO NA VIFAA.

Kwa kuwa mjenzi anajitegemea kwa kila kitu suala la gharama za kujikimu linategemea sana muda. Hivyo upatikanaji wa fedha za malipo kwa watenda kazi ni muhimu. Endapo kazi itasimama kwa sababu zilizosababishwa na TAWA, Mjenzi atachukua moja ya hatua zifuatazo:

(a) Atamuarifu msimamizi juu ya hali hiyo.
(b) Atasimamisha kazi kwa muda.

## I. KUCHELEWESHA KAZI.

Endapo kutatokea ucheleweshaji wa kazi kwa sababu ambazo hazitokani na ucheleweshaji wa TAWA, Mjenzi atawajibika kulipa malipo yake kiasi cha shilingi 10,000 kwa kila siku mpaka kazi itakapokamilika.

## J. MGOGORO.

Endapo kutatokea mgogoro wakati wa utekelezaji wa kazi hii, pande zote mbili za mkataba tunakubaliana kwamba tutatafuta usuluhishi kutoka ndani ya jumuia ya watu wa ujenzi na au taasisi za ujenzi ili kumaliza tatizo husika.

## K. KUSITISHA MKATABA

Mkataba huu unaweza kusitishwa iwapo upande wowote utaonekana kutotimiza makubaliano yaliyofikiwa ikiwa ni pamoja kufanya kazi kwa kiwango cha chini kuliko ilivyotarajiwa. Ikiwa Mkataba utasitishwa pande husika italazimika kulipa tozo iliyoainishwa kwenye Ibara I hadi tarehe ya kusitishwa kwa Mkataba huu.

## L. SHERIA ZITAKAZOTUMIKA PAMOJA NA MAHAKAMA ZENYE MAMLAKA

Mkataba huu utasimamiwa na Sheria za Tanzania na Mahakama za Tanzania zitakuwa na Mamlaka ya kusikiliza Shauri litakalotokana na Mkataba huu.

Kwa kuthibitisha makubaliano haya tunaweka sahihi zetu hapa.

**Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori**

SAHIHI..........................................

JINA SAID DIWANI MSHANA

CHEO MHIFADHI MSIMAMIZI/MKUU WA PORI

**USHAHIDI**

SAHIHI..........................................

JINA HASHIMU SAID NGULI

CHEO MHASIBU MSAIDIZI

**KWA MJENZI**

SAHIHI..........................................

JINA GEORGE ETIENNE MPONDA

CHEO FUNDI MKUU

**SHAHIDI WA MJENZI**

SAHIHI..........................................

JINA RAMADHANI ALLY AMISI

CHEO FUNDI

MWISHO.

GEORGE ETIENNE MPONDA
S.L.P 121
MASASI –MTWARA
0713 248505/0767248505
30/12/2021

KAIMU KAMISHINA
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA-TAWA
S.L.P 2658
MOROGORO

**YAH :MAKUBALIANO YA KUFANYA KAZI KWA KIASI CHA SHILINGI MILLIONI ISHIRINI NA MOJA TU (21,000,000) KWENYE CAMPSITE LUKWIKA LUMESULE.**

Rejea somo tajwa hapo juu

Leo tarehe 30/12/2021 tulikuwa na kikao kuhusu kazi tajwa hapo juu baada ya majadilino Nimekubali kufanya kazi kwa kiasi tajwa hapo juu .

Ni matumaini yangu kuwa endapo vifaa vyote vitakuwa site nitafanya kazi hiyo kwa kipindi cha mwezi mmoja na kukamilisha.

Natanguliza shukrani zangu za dhati

NAOMBA KUWASILISHA

......................................

GEORGE ETIENNE MPONDA